KWA JINA LA ALLÂH , MWINGI WA REHEMA, MWENYE KUREHEMU

25/= Ksh

Al-Hudaa [Uongofu]

الهدى

Volume 16, Issue 4

29th Dhul Hijjah 1432

25th Nov, 2011

YALIYOMO

SWADAKA ZA ... 1

SHEREHE YA ASHOORA 2 - 4

SWADAKA ZA MASHI'AH [HUSSEINIYYAH]

Na: Shaykh al-'Allaamah 'Abd al-'Azeez ibn 'Abd-Allaah ibn Baaz (رحمه الله)

SUALI: Ni nini hukmu ya Pote la al-Husseiniyya miongoni mwa ma-Raafidhee na yale mambo yanayofanywa hapo kama vile kujipiga makofi na kujinyafura nyuso, kuomboleza, mtu kupasua nguo zake na kujipiga makonde, mara nyengine kwa kutumia silisili, na huku wakiwalingania waliokufa pamoja na Ahl al-Bayt (jamii ya nyumba ya Mtume) wawanusuru?

JAWABU 1: Kila Slfa Njema ni yenye kumstahiki Allaah (Alhamdulillaah).

Hili ni jambo Ovu mno na bid'ah inayostahiki kukemewa vikali kabisa na kuepukwa. Hairuhusiwi mtu kujumuika hapo au kula chakula kinachotolewa kwenye mikusanyiko hii kwa sababu Mtume (صلى الله عليه وسلم) na Maswahaba zake (رضي الله عنهم) miongoni mwa Ahl al Bayt na wengineo hawakufanya hayo.

Amesema Mtume (صلى الله عليه وسلم): "Yoyote mwenye kuzua katika jambo letu hili (Uislamu) chochote kisichokuwa katika sehemu yake kitakataliwa mbali". [Bukhari na Muslim].

Na akasema Mtume (صلى الله عليه وسلم): "Yoyote mwenye kuzua jambo lisilokuwa na uhusiano na jambo letu hili [Uislamu] atarudishiwa mwenyewe." [Imepokewa na Muslim katika Swaheeh yake, na imepokewa na al-Bukhaari (رضي الله عنهم) katika Swaheeh yake, mu'allaq majzoom]. Na kuna ahaadeeth nyingi zenye maana kama hiyo. Ama kuhusu kuomba msaada kwa waliokufa na Ahl al Bayt, hiyo ni sampuli ya Shirk Kubwa kulingana na muafaka wa wanavyuoni kwa sababu Allaah amesema (tafsiri yenye maana): **"Na anayemuabudu – pamoja na Allaah – mungu mwengine, yeye hana dalili ya (jambo) hili; basi bila shaka hisabu yake iko kwa Mola wake. Kwa hakika makafiri hawafanikiwi."** [al-Mu'minoon 23:117].

"Na kwa hakika misikiti (yote) ni ya Allaah, basi musimuabudu yoyote pamoja na Allaah." [al-Jinn 72:18]

"Na wapotofu (wapotevu) wakubwa ni nani kuliko wale wanaowaomba asiyekuwa Allaah ambao hawatawajibu mpaka siku ya Kiyama, na hawatambui dua zao. Na (ambao) watakapokusanywa watu watakuwa maadui zao, na wataikataa ibada yao." [al-Ahqaaf 46:5-6].

"Anauingiza usiku katika mchana na kuuingiza mchana katika usiku, na Amevitiisha Jua na Mwezi; vyote (vinakwenda mchana na usiku) mpaka muda maalum ufike. Huyo ndiye Allaah, Mola wenu, Mwenye Ufalme; na wale mnaowaabudu kinyume Chake, wao hawamiliki hata utando (ugozi) wa kokwa ya tende! Kama mkiwaomba (masanamu hao), hawasikii wito wenu; na hata kama wakisikia hawatakujibuni (kwani hawana uweza wowote); na siku ya Kiyama watakataa ushirikina wenu. Wala (yoyote) hatakuambia kama (Aambiwavyo Allaah) - Mjuzi wa kwelikweli." [Faatir 35:13-14]

Na kuna ayaat nyingi zenye maana kama hizo. Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: "Du'aa' (maombi) ni sampuli ya ibada." (Imepokewa na waandishi wanne wa Sunan kwa isnaad swaheeh). Na Muslim amepokea kwenye swaheeh yake kutoka kwa Ameer al-Mu'mineen 'Ali ibn Abee Twaalib (رضي الله عنه) yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: "Amelaaniwa mwenye kuchinja kwa ajili ya yoyote asiyekuwa Allaah."

Kilicho waajib juu ya ma-Shi'ah wote na mtu mwengine yoyote ni kumuabudu Allaah Peke yake kwa ikhlaas, na kujitahadhari, na kutahadhari kumnyenyekea yoyote asiyekuwa Allaah kwa kuomba msaada, au kuwaomba waliokufa au walio mbali nasi, iwe ni miongoni mwa Ahlu al-Bayt au wengineo.

Vilevile ni waajib kujiepusha kuwaomba au kutaka msaada kutoka kwa vitu visivyokuwa na roho, kama vile masanamu, nyota na kadhaalika juu ya msingi huohuo wa kisheriya (dalili) tulioutaja hapo awali.

Wanavyuoni wa Ahlus-Sunnah wal Jamaa'ah, na wa Maswahaba na wengineo, wamekubaliana kwa muafaka juu ya mas'ala haya.

JAWABU 2: Ni nini hukmu ya swadaka zinazotolewa kwenye sehemu hizo katika siku hizo? Ni nini hukmu ya vinywaji vinavyogawanywa kwenye mabarabara na kwa watu wa njiani?

Jawabu la suali hili ni sawa na jawabu la suali la kwanza, ambalo ni bid'ah iliyolaumiwa vikali na hairuhusiwi kushiriki kwa njia yoyote, au kula nyama za swadaka hizo, au kunywa vinywaji vyovyote. Ikiwa swadaka zilikusudiwa kwa yoyote asiyekuwa Allaah kutokana na miongoni mwa Ahl al-Bayt au mtu yoyote, hii ni Shirk Kubwa kwa sababu Allaah amesema (tafsiri yenye maana): **"Sema: "Hakika swala yangu, na ibada zangu (zote nyengine) na uzima wangu, na kufa kwangu; (zote) ni kwa Allaah. Mwumba wa walimwengu wote. (Likinisibu jambo limenisibu kwa kutaka Allaah si kwa kutaka viumbe vyake. Na yote ninayofanya nayafanya kwa ajili yake)."** [al-An'aam 6:162-163]

"Hakika Tumekupa (wewe Muhammad) Al-Kawthar (mto wa Peponi). Basi swali kwa ajili ya Mola wako na uchinje." [al-Kawthar 108:1-2]

Na kuna ayaat nyingi na ahaadeeth zenye maana sawa na hizi.

Twamuomba Allaah atsahilishie sote pamoja na Waislamu wote tufanye kila alipendalo na kumridhisha Yeye, na atuhifadhi sote na pepesi za upotofu, kwani Yeye ndiye aliyekaribu nasi na daima yuko tayari kutusikiza.

KUSHEREHEKEA 'AASHOORA' NA KUIFANYA KUWA NI SIKU YA MAOMBOLEZI

Na: Ibn Taymiyyah - Fataawa al-Kubra Prt. 5]

"Ni nini hukmu kuhusu mambo wanayofanya watu katika siku ya 'Aashooraa', kama vile kutia wanja machoni, kuoga, kutumia henna, kupeana mikono kwa maamkuzi, kupika tangalizi, kuonyesha furaha zao na mengine kama hayo? Je, kuna hadeeth yoyote iliyo swaheeh iliyopokewa kutoka kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) au laa? Ikiwa hakuna hadeeth iliyo swaheeh kwenye mas'ala hayo, kufanya mambo hayo itakuwa ni bid'ah au laa? Je kuhusu mambo mengine yanayofanywa na watu, kama vile kuomboleza, kuwa na huzuni, kususia chakula, taabini, kulia kwa makelele, kurarua nguo zao, na kadhaalika, kuna dalili yoyote ya kujuzisha hayo?"

Sheikh ul Islaam Ibn Taymiyyah (رحمه الله) aliulizwa suala hilo, nae akajibu kama ifuatavyo:

Alhamdulillaah, hakuna chochote kama hicho kilichopokewa kwenye hadeeth zilizo swaheeh kutoka kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) au kutoka kwa Maswahaba zake. Hakuna miongoni mwa ma-Imaam wa Waislamu aliwahi kuhimiza au kupendekeza mambo kama hayo, wala si ma-Imaam wanne na wala si wowote miongoni mwao. Hakuna mwanachuoni yoyote vmwenye kutegemewa aliyewahi kupokea mambo kama hayo, si kutoka kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم), wala kutoka kwa Maswahaba, wala kutoka kwa ma-Taabi'een; wala si kwenye riwaya iliyo swaheeh wala hata riwaya iliyo dha'eef. Wala hayapatikani hayo kwenye vitabu vilivyo swaheeh wala vitabu vya Sunan, wala si kwenye vitabu vya musnad. Hapakuwahi kujulikana sampuli ya hadeeth kama hiyo katika zama za karne zilizokuwa ni bora, lakini baadhi ya wapokezi waliokuja baadae ndio waliopokea ahaadeeth kama ile moja isemayo, "Yoyote mwenye kutia wanja kwenye macho yake katika siku ya 'Aashooraa', basi hatopata maradhi ya macho katika mwaka huo, na yoyote mwenye kuoga katika siku ya 'Aashooraa', basi hatokuwa mgonjwa katika mwaka huo mzima," na kadhaalika. Vilevile wamepokea riwaya kuhusiana na madai ya fadhla za kuswali katika siku ya 'Aashooraa', na riwaya nyengine zinazosema yakwamba katika siku ya 'Aashooraa', Adam (عليه السلام) alitubia, Jahazi ya Mtume Nuh (عليه السلام) ilitulia kwenye Mlima wa Judiyy, Mtume Yusuf (عليه السلام) alirudi kwa babake Ya'qoob (عليه السلام), Mtume Ibraahim (عليه السلام) aliokolewa kutokamana na moto, kondoo alitolewa au alipewa kuwa ni swadaka badala ya Mtume Ismaa'il (عليه السلام) na kadhaalika. Vilevile wamepokea hadeeth ya urongo iliyozuliwa eti kutoka kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) yakwamba, "Yoyote aliye mkarimu kwa ahli yake katika siku ya 'Aashooraa', Allaah Atakuwa na Ukarimu nae katika muda uliobaki wa mwaka huo."

(Kisha Ibn Taymiyyah akayajadili mapote mawili ya upotofu yaliyokuwepo mjini Kufa katika nchi ya Iraaq, na yote yameufanya mwezi wa 'Aashooraa' kuwa ni siku kuu kwa ajili ya bid'ah zao).

Pote la ma-Raafidha wakajifanyia kwa kudhihirisha kutoa bay'ah zao za utwi'ifu kwa Ahl al Bayt, ingawa kwa siri walikuwa ni emma wazushi na makafiri au wajinga wakawa wanakwenda kwa matamaniwa ya nafsi zao.

Pote la Naasibi lilikuwa likimchukia 'Ali na Maswahaba zake kwa sababu ya matatizo na mauaji yaliyowahi kutokea. Imepokewa kwenye swaheeh Muslim yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: "Miongoni mwa (kabila la) Thaqeef kutakuwepo na mtu mrongo na mwenye kudhulumu na kuwakandamiza watu." Mrongo huyo alikuwa ni al-Mukhtaar ibn Abi 'Ubayd al-Thaqafi, ambae aliyedhihirisha kutoa bay'ah yake ya utwi'ifu na kuwaunga mkono Ahl al Bayt, na akamuuwa 'Ubayd-Allaah ibn Ziyaad, aliyekuwa ni kiongozi wa Iraaq, na ndiye aliyewaandaa kundi lililomuuwa al-Hussein Ibn 'Ali (رضي الله عنهم); kasha (al-Mukhtaar) akamtangaza waziwazi yakwamba alikuwa ni mrongo, kwa kudai yakwamba ati yeye alikuwa ni Mtume na kwamba Jibreel (عليه السلام) alimletea wahyi. Watu wakawaeleza Ibn 'Umar na Ibn 'Abbaas kuhusu tukio hilo, na wakasema kumwambia mmoja wao, "al-Mukhtaar ibn Abi 'Ubayd anadai kuwa yeye ni Mtume [annahu yanzilu 'alayhi]." Akasema, "Amesema kweli, kwani Allaah amesema (tafsiri yenye maana): **"Je, nikuambieni ambao mashetani wanawateremkia."** [al-Shu'ara' 26:221]." Wakasema kumwambia mwengine: "Al-Mukhtaar anadai yakwamba anapata wahyi." Akasema, 'Naam, anasema kweli'. **"Na hapana shaka yakwamba mashetwani wanawafunulia marafiki zao (miongoni mwa wana-adamu) kubishana nanyi (katika mambo namna haya yasiyokuwa na maana). Na kama mkiwatwi'i, mtakuwa washirikina."** [al-An-aam 6:121]. Tafsiri yake ni kwamba, 'Kama ambavyo Yusuf ath-Thaqafee, aliyekuwa ni mpinzani mkubwa wa Ali na wenzake. Al-Hajjaaj alikuwa ni Naasibi na al-Mukhtaar alikuwa ni Raafidhee, na Raafidhee huyualikuwa ni mrongo mkubwa na mwenye hatia zaidi ya kuzua na kueneza uvumi, kwa sababu alidai kuwa yeye ni Mtume.

Paliwahi kuwa na vita vikubwa baina ya makundi haya mawili katika mji wa Kufa, wakati al-Hussein bin Ali (رضي الله عنه) alipouwawa katika siku ya 'Aashooraa', nae aliuwawa na kundi ovu la ki-dhaalim. Allaah akamja'alia al-Hussein kifo cha Shaheed, kama alivyowaja'alia baadhi nyengine ya jamii yake, aliinyanyua daraja yake, kama alivyowapa daraja ya juu kina Hamzah, Ja'far, babake Ali na wengineo. Al-Hussein na nduguye al-Hassan ni viongozi wa vijana huko Peponi. Daraja ya juu hupatikana kutokana na mateso kama alivyosema Mtume (صلى الله عليه وسلم), pindi alipoulizwa ni wapi watu watakaoteseka zaidi. Akasema, "Ni Mitume, kisha ni watu wema, kisha ni watakaofuata kwa wema, na wengine watakaowafuata hao kwa wema. Mtu atateswa kulingana na daraja yake ya Imaan. Iwapo Imani yake itakuwa ni ya kisawasawa, atateseka zaidi, lakini iwapo imani yake haitokuwa thabiti, mateso yake hayatokuwa makubwa. Mu'min ataendelea kuteseka mpaka awe anatembea juu ya ardhi hii akiwa hana madhambi." (Imepokewa na at-Tirmidhi na wengineo).

Al-Hassan na al-Hussein wametekeleza waliyoyatekeleza na wakafika daraja ya juu waliyofika kwa usaidizi na makadirio ya Allaah. Hawakupata mateso makubwa kuwashinda mababa zao, kwani wao walizaliwa na kulelewa kwenye zama zilizokuwa bora za Uislamu na Waislamu wakawaheshimu na kuwatukuza. Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikufa wao wakiwa ni watoto wadogo, na Allaah akawabariki kwa kuwafanyia mitihani kwa hali ambayo itakayowafanya daraja zao ziwafikie jamii zao waliowatangulia kama za wale waliokuwa na daraja za juu kuliko wao. Ali Ibn Abee Twaalib alikuwa ni mbora kuliko wao, nae akauwawa kama shaheed. Mauaji ya al-Hussein ni miongoni mwa mambo yaliyoleta fitna miongoni mwa watu, kama yalivyokuwa mauaji ya 'Uthmaan ambayo ndiyo yaliyokuwa miongoni

(Endelea Kwenye Ukurasa wa 3)

(Endelea kutoka Ukurasa wa 2)

mwa sababu za fitna kubwa, kwa sababu ya mambo yaliyougawanya Umma mpaka leo. Kwahiyo Mtume (صلى الله عليه وسلم) akasema: “Kuna mambo matatu ambayo mtu yoyote atakayoepushwa nayo, basi atakuwa ameokolewa: Kifo changu, mauaji ya khalifa mwenye subira na ad-Dajjaal.” Sheikh ul Islaam (رحمه الله) alitaja kwa mukhtasar kuhusu wasifu wa al-Hassan na tabia yake njema, kasha akasema: “Kisha akafa, na Allaah alikuwa radhi nae na akampa taadhima kubwa. Baadhi ya makundi yalimuandikia al-Hussein na kumuahidi kumsaidia iwapo ataendelea na kujitangaza kuwa yeye ni khalifa, lakini hawakuwa ni wakweli. Al-Hussein alipompeleka binamu yake [mtoto wa Ami yake] kwao, walivunja ahadi yao na kumsaidia aliyekuwa adui wao, na wakapigana nae dhidi ya binamu yake [mtoto wa Ami yake]. Wale waliokuwa na busara na waliokuwa wakimpenda al-Hussein, kama vile Ibn Abbaas na Ibn Umar na wengineo, walimnasihi asende kwao, na asikubali ahadi zozote. Walidhania yakwamba kwenda kwake kuonana nao hakutokuwa na maana yoyote na kwamba matokeo hayatokuwa mazuri. Mambo yakageuka kama jinsi walivyosema, na hivyo ndivyo ambavyo Allaah alivyokadiria yatokee. Pindi al-Hussein (رضي الله عنه) alipotokeza na kujionea mwenyewe yakwamba mambo si kama alivyotarajia, aliwataka wamuache ili arudi zake, au wamuache ajiunge na jeshi linalotetea kulinda mipaka ya Uislamu, au aungane na binamu yake Yazeed, lakini hawakukubali kumuacha afanye chochote katika aliyotaka isipokuwa ajisalimishe kwao na awe kama mfungwa. Basi akapambana nao, na wakamuuwa pamoja na wenzake aliokuwa nao, na hatimae wakamuuwa (kwa kumkata kichwa chake), kwahivyo akafa kama shaheed, ambaye ushahidi wake ukamletea Utukufu kutoka kwa Allaah, na kwahiyo akajumuika pamoja na jamii nzuri iliyokuwa na heshima kubwa. Mauaji yake yakaleta aibu kubwa kwa wale waliomuuwa kwa njia ya dhulma, na kuleta uharibifu mkubwa miongoni mwa watu. Kundi la wajinga, upotofu ambao ni emma wazushi au wanafiki, au wapotofu au waliopotezwa – waliodhihirisha bay’ah (kumuunga mkono) na jamii yake na watu wa nyumba yake, kwahiyo wakaichukuwa siku ya ’Aashooraa’ kama siku ya maombolezi na vilio, ambamo ndani yake hudhihirisha mila za ki-Jaahiliyyah, kama vile kujipiga makofi na kujipasulia nguo zao, wakiomboleza kulingana na mila za ki-Jaahiliyyah. Lakini aliyotuamrisha Allaah pindi misiba itufikapo – pale wakati maafa hayo yatokeapo, ni kuyachukulia kwa kusubiri na kuvumilia, na kutarajia malipo mema na kukumbuka yakwamba mambo yote yanakuja kutoka kwa Allaah na ni lazima turudi Kwake kama alivyosema (tafsiri yenye maana): **“Na wapashe habari njema wanaosubiri. Ambao uwapatapo msiba husema: ‘Hakika sisi ni wa Allaah, na kwake Yeye tutarejea’. Hao juu yao zitakuwa baraka zitokazo kwa Mola wao na rehema; na ndio wenye kuongoka.”** [al -Baqarah 2:155-157].

Imepokewa kwenye swaheeh yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: “Si katika sisi yule mwenye kujitwanga makofi, kupasua nguo zake na kuomba maombi ya ki-Jaahiliyyah.” Na akasema: “Mimi sina fungu lolote na wale wenye kujitwanga makofi [kwenye nyuso zao], kunyoa [vichwa vyao] na kurarua [nguo zao].” Na akasema: “Iwapo mwanamke anayeomboleza kwa kilio hatotubia kabla ya kufa kwake, ataletwa siku ya Kufufuliwa akiwa amevishwa Surwale ya Lami na shati lenye kigaga.”

Katika al-Musnad, imepokewa kutoka kwa Faatimah bint al-Hussein, kutoka kwa babake, al-Hussein, yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: “Hapana mtu yoyote atakaepata msiba, na mara tu atakapoukumbuka, hata kama ni wa zamani, yeye husema, ’Inna lillaahi wainna ilayhi raaji’oon’, isipokuwa Allaah atamlipa wema ulio sawa na alivyomlipa pindi alipoupata msiba huo.” Hivi ndivyo jinsi Allaah anavyowaenzi waumini. Ikiwa msiba uliomsibu al-Hussein, na misiba mengine, yanatajwa baada ya muda wote huu, wao na waseme ’Inna lillaahi wainna ilayhi raaji’oon’. Kama Allaah na Mtume wake walivyotuamrisha, ili tupate kulipwa wema kama ule uliopatikana katika siku ya msiba wenyewe ulipotokea. Ikiwa Allaah ametuamrisha tuwe na subira na uvumilivu na tutarajie malipo wakati wa msiba unapotokea, je baada ya kupita muda mrefu? Sheitwaan amelifanya jambo hili kuwa ni lenye kuvutia kwa waliopotezwa, kwahiyo wakaichukulia siku ya ’Aashooraa’ kuwa ni siku ya maombolezi, wanapo omboleza na kulia kwa makelele, wakasoma mashairi ya kuomboleza na wakatoa visa vya urongo. Hata kukawa na ukweli kwenye visa hivyo, utakuta yakwamba hakuna malengo mengine isipokuwa ni kuyakariri maombolezi ya kikundi chao, na kuchochea matukio na uhasama miongoni mwa Waislamu, wakiwakashifu na kuwalaani wanaokuja mbele yao, na wakaeleza urongo mtupu, na wakaleta matatizo mengi ulimwenguni.

Mapote mengi ya Uislamu hayajawahi kujua pote lolote lenye kueneza urongo mwingi au kusababisha uhasama mkubwa au kuwasaidia makafiri dhidi ya Waislamu kuliko pote hili la upotofu lenye uovu mkubwa. Hawa ni waovu zaidi hata kuliko ma-Khawaarij, waliotokomea nje ya boma la Uislamu. Wao ndio wale ambao Mtume (صلى الله عليه وسلم) aliotuambia kuwahusu: “Watawauwa Waislamu na kuwawacha watu wenye kuabudu masanamu.” Kundi hili lilishirikiana na Mayahudi, Makristo na Mushrikeen dhidi ya jamii ya nyumba ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) na Ummah wake wa Waumini, na pia waliwasaidia washirikina wa ki-Turki na Tar-tar kufanya waliyoyafanya huko Baghdad, na kwengineko kwa vizazi vya Mtume (صلى الله عليه وسلم). Yaani; watawala wa Abbaasiyya na wengineo, na waumini; Waturuki na Tar-tar wakawauwa, wakawafanya wanawake zao kuwa watumwa na kuharibu majumba yao. Uovu na madhara wanayowafanyia Waislamu hayawezi kukadiriwa na mtu yoyote, bila ya kujali ushawishi wao wa ki-mazungumzo. Baadhi yao nyengine – emma ma-Naasibi wanaopinga na kuwa na uadui na al-Hussein na jamii yake au watu wajinga wanaojaribu kuondoa uovu kwa kutumia uovu, ufisadi kwa kutumia ufisadi, urongo kwa kutumia urongo, bid’ah kwa kutumia bid’ah - wanayapinga kwa kutumia riwaya za kuzua kwa kuwapendelea kuifanya siku ya ‘Aashooraa’ kuwa ni siku ya sherehe, kwa kutia wanja machine, na henna, kugharimika kwa kuwafurahisha watoto, kupika vyakula maalum na mambo mengine yenye kufanywa katika siku za ‘Eid na matukio maalum. Watu hawa wameichukulia siku ya ‘Aashooraa’ kuwa ni kama siku kusherehekea kama ‘Eid, haliyakuwa wengine wameichukulia kuwa ni siku ya maombolezi. Wote hao wako kwenye makosa, na wote wanakwenda kinyume cha Sunnah, hata kama kundi jengine (ma-Raafidha) ni waovu zaidi katika niya zao na ni wajinga zaidi na kuwa wazi zaidi kwenye makosa ... Lakini Allaah anatuamrisha sisi kuwa na uadilifu na tuwatendee wengine usawa. Amesema Mtume (صلى

(Endelea kutoka Uk. 3)

(صلى الله عليه وسلم): “Wale ambao miongoni mwenu watakaoishi zaidi, baada ya kufa kwangu wataona migogoro mengi. Nawahimiza kushikamana na Sunnah zangu na sunnah za Makhalifa wangu waongofu (al-khulafa’ al-raashidoon) watakaokuja baada yangu. Shikamaneni nazo kana kwamba mumeuma kwa Magego yenu (meno ya mwisho - yenye nguvu). Na mujitahadhari na mambo ya kuzua, kwani kila la kuzuliwa ni upotofu, na kila upotofu.” Si Mtume (صلى الله عليه وسلم) wala si Makhalifa waongofu (khulafa’ al-raashidoon), waliofanya mambo hayo katika siku za ‘Aashooraa’. Hawakuifanya kuwa ni siku ya kuomboleza wala siku ya kusherehekea.

Lakini, siku Mtume (صلى الله عليه وسلم) alipokuja Madina, aliwakuta Mayahudi wakifunga katika siku ya ’Aashooraa’. Akasema, ‘Kuna nini?’ Akaambiwa, ’Hii ni siku ambayo Allaah alimuokoa Musa na kuzama, kwahiyo sisi twafunga siku hii’. Akawaambia, ’Sisi tuna haki zaidi kwa Musa kuliko nyinyi’. Kwahiyo akafunga siku hiyo, na akawaamrisha Waislamu wafinge katika siku hiyo.’

Ma-Quraysh vilevile walikuwa wakiiadhimisha siku hiyo katika zama za Jahiliyyah. Siku ambayo watu walipoamrishwa kufunga ilikuwa ni siku moja peke yake. Wakati Mtume (صلى الله عليه وسلم) alipokuja Madina, ilikuwa ni Rabee’ ul Awwal na mwaka uliofuata akafunga siku ya ‘Aashooraa’ na akawaamrisha watu wafunge. Kisha katika mwaka huo, kufunga saumu ya mwezi wa Ramadhaan ikafaradhishwa na kufunga saumu ya ‘Aashooraa’ ikafutwa. Wanavyuoni wakajadiliana iwapo kufunga katika siku hiyo (’Aashooraa’) ilikuwa ni waajib au Mustahabb. Mtume (صلى الله عليه وسلم) hakuwaambia Waislamu wa kawaida kufunga katika siku ya ‘Aashooraa’, lakini alikuwa akisema: “Hii ni siku ya ‘Aashooraa’, mimi nafunga katika siku hii, na yoyote atakae kufunga katika siku hii, anaweza kufunga.” na akasema: “Kufunga katika siku ya ‘Aashooraa’, hufuta madhambi ya mwaka mzima na kufunga siku ya ‘Arafah hufuta madhambi ya miaka miwili”. Alipofikia mwishoni mwa maisha yake, Mtume (صلى الله عليه وسلم) alisikiya yakwamba Mayahudi wameifanya siku ya ‘Aashooraa’ kuwa ni siku ya Furaha, akasema, “Ikiwa nitakuwa hai mwaka ujao, kwa hakika mimi nitafunga siku ya tarehe Tisa” - ili niwe ni mwenye kuwakhalifu Mayahudi, na nisiwe ni mwenye kufanana nao katika kuifanya siku hiyo kuwa ni ya kusherehekea.

Kulikuwa na baadhi ya Maswahaba na wanavyuoni ambao hawakufunga katika siku hiyo na hawakuichukulia kuwa ni siku iliyopendekezwa (mustahabb), lakini wakadhania yakwamba ilikuwa ni makrooh kuipwekesha siku hiyo kwa kufunga. Haya yamepokewa na kundi la watu wa Koofa (wanavyuoni wa Koofa). Baadhi ya wanavyuoni wengine wamesema yakwamba ni mustahabb kufunga siku hiyo. Kauli ya sawa ni kwamba ilikuwa ni mustahabb kwa mwenye kufunga siku ya ’Aashooraa’ afunge tarehe Tisa (ya Muharram) vilevile, kwa sababu hii ilikuwa ni amri ya mwisho ya Mtume (صلى الله عليه وسلم), kama alivyosema, “Ikiwa nitakuwa hai mwaka ujao, kwa hakika mimi nitafunga siku ya tarehe Tisa, pamoja na Kumi.” [haya yamepokewa kwa isnaad tafauti tafauti. Haya ndiyo yaliyopendekezwa kwenye Sunan za Mtume (صلى الله عليه وسلم)].

Amma kuhusu mas’ala mengine, kama vile mapishi ya sampuli mbalimbali, au kuvaa nguo mpya, au kugharimika kwa kuwafurahisha jamii nzima, au hata kununua vyakula vya mwaka mzima katika siku hiyo, au kufanya Ibada maalum kwa ajili ya siku hiyo, kama vile swala maalum, au kukusudia kuchinja mnyama katika siku hiyo, au kuweka sehemu za swadaka za nyama na kufanya mapishi maalum, au kutia wanja machoni na kutia henna, au kuoga, au kupeana mikono na kupongezana, au kutembeleana, au kutembelea misikiti au mash-had (majumba ya ibada za ushirikina) na kadhaalika. Yote hayo ni miongoni mwa bid’ah zenye kulaumika vikali na ni mambo ya makosa.

Hapana katika hayo, chenye kuhusiana na Sunnah za Mtume (صلى الله عليه وسلم) au njia ya khulafaa’ ar-Raashidoon. Hayakupasishwa hayo na Imaam yoyote wa Waislamu, si Maalik, si Ath-Thawree, si al-Layth Ibn Sa’d, wala Abu Haneefah, wala si al-Awzaa’i, wala si ash-Shaafi’ee, wala si Ahmad Ibn Hanbal, wala si Is-haaq ibn Ar-Raahaway, wala si yoyote miongoni mwa ma-Imaam wa Waislamu.

Dini ya Uislamu imejengwa juu ya misingi miwili: yakwamba hatufai kuabudu chochote asiyekuwa Allaah Peke Yake, na kwamba tumuabudu Yeye kulingana na jinsi alivyotufunza, na wala sio kwa njia za bid’ah au bid’ah potofu. Amesema Allaah (tafsiri yenye maana): **“.. anayependa kukutana na Mola wake na afanye vitendo vizuri wala asimshirikishe yoyote katika ibada ya Mola wake.”** [al-Kahf 18:110].

Matendo mema ni yale yanayopendwa na Allaah pamoja na Mtume wake, yale yaliyofaradhishwa na Uislamu na kwenye Sunnah. Kwahiyo, ‘Umar ibn al-Khattaab (رضي الله عنه) alikuwa akisema kwenye Du’a’ yake: “Yaa Allaah zija’aliye amali zangu kuwa ni nzuri na uzitakase kwa ajili yako, na wala usija’aliye kuwepo na fungu la yoyote au kitu chochote ndani yake.”

(Hayo ni katika Mukhtasari wa maneno ya Sheikh ul Islaam Ibn Taymiyyah (رحمه الله). Al-Fataawa al-Kubra, Sehemu ya 5). Na Allaah ndiye Mwenye kuongoza kwenye Njia ya sawa.

NENO LA BUSARA

Amepokea Anas (رضي الله عنه): “Siku moja tulikuwa pamoja na Mtume (صلى الله عليه وسلم) tulipomuona na sura za furaha, akatwambia, “mwajua ni kwa nini mimi nina furaha?” Tukasema, “Allaah na Mtume wake ndiwo wajuzi zaidi wa hayo.” Basi akasema, “nilikuwa nikifikiri kuhusu mjadala ambao mja atakaokuwa nao na Mola Wake. Atasema, “Ewe Mola wangu, si wewe umeniahidi ulinzi dhidi ya maonevu?” Atasema, “Naam.” Kisha Yule mja atasema, Mimi sitokubali ushahidi wowote dhidi yangu isipokuwa kutoka kwangu mimi mwenyewe.” Atasema, “Ushahidi dhidi yako kutoka kwako utatosheleza, pamoja na ule wa Malaika wawili waliochaguliwa wahifadhi matendo yako.” Kisha mdomo wake utafungwa na mikono yake pamoja na miguu yake itaulizwa izungumze na itasema kuhusu aliyoyafanya. Kisha mdomo wake utaachwa uzungumze na utasema, “Ewe mjinga mkubwa! La’ana ya Allaah ikushukie! Mimi nilikuwa najaribu kukuhifadhi.””

Muslim 18/104-105